JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

MATOKEO YA RUFAA ZILIZOPOKELEWA TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI KWA AJILI YA UCHAGUZI

MDOGO WA TAREHE 16 SEPTEMBA, 2018

Na	HALMASHAURI	KATA	MRUFANI		MRUFANIWA		MAAMUZI YA TUME	*SABABU*
			JINA	CHAMA	JINA	CHAMA		
1	WILAYA YA KYELA	NKUYU	LUSAJO LUKASI MWAKANANGE	CHADEMA	KAINI ALEXANDER MWAKANY'EMBE	CCM	Rufaa imekubaliwa na Mrufaniwa amerejeshwa kuwa mgombea Udiwani katika Kata ya Nkuyu.	*Tume imejiridhisha kuwa Fomu Na. 8C, Sehemu A, Kipengele cha 7 Mrufani amekata neno NDIYO na katika sehemu C na D amekata neno Bibi na Bi, hivyo fomu hiyo imejazwa ipasavyo.*
2	JIJI LA MBEYA	SISIMBA	GEOFREY KAJIGILI MWANDUMBYA	CCM	ORDINARY MICHAEL SANGA	CHADEMA	Rufaa imekubaliwa na Mrufaniwa ameondolewa katika orodha ya Wagombea Udiwani katika Kata ya Sisimba.	*Kwa mujibu wa kanuni ya 25 ya Kanuni za Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015 mgombea anatakiwa kujaza Fomu ya uteuzi kwa ukamilifu. Aidha, katika Fomu yake ya uteuzi Na. 8C Sehemu A kipengele cha 7 kinachohusu taarifa binafsi za mgombea kutoa maelezo iwapo amewahi kushitakiwa na kuhukumiwa kwa kosa la jinai, mrufaniwa amekata neno NDIYO, akimaanisha kuwa hakuwahi kushtakiwa kwa kosa la jinai.* *Kwa mujibu wa barua yake ya tarehe 25 Agosti, 2018 katika utetezi wake wakati wa pingamizi mrufaniwa aliandika na alikiri kuwa aliwahi kuhukumiwa na kufungwa. Katika mazingira hayo, mrufaniwa ameshindwa kujaza Fomu ya uteuzi kwa mujibu wa kanuni ya 25 ya kanuni tajwa, hivyo amepoteza sifa ya kuteuliwa kuwa mgombea.* *Kama mrufaniwa angeeleza kwamba aliwahi kutiwa hatiani kwa kosa la jinai, kusingemuondolea sifa ya kuteuliwa kugombea Udiwani kwakuwa kosa lililomtia hatiani halimuondolei sifa ya kuwa mgombea.*
3	JIJI LA MBEYA	MAANGA	NEWTON MWASABWITE MWATUJOBE	CCM	STEVEN GRISTON MWASHILINDI	CHADEMA	Rufaa imekataliwa na Mrufaniwa anaendelea kuwa Mgombea Udiwani katika Kata ya Maanga.	*Tume imepitia Fomu ya uteuzi ya Mrufaniwa na kujiridhisha kuwa kipengele C cha Fomu za uteuzi kimejazwa kikamilifu na kugongwa muhuri wa Katibu Wilaya ya Mbeya Mjini wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, kwa mujibu wa kanuni ya 25 ya Kanuni za Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015.*

Na	HALMASHAURI	KATA	MRUFANI		MRUFANIWA		MAAMUZI YA TUME	*SABABU*
			JINA	CHAMA	JINA	CHAMA		
4	JIJI LA MBEYA	NSALAGA	DAUDI NELSON NGOGO	CCM	REWARD WILLIAM MSHANGA	CHADEMA	Rufaa imekataliwa na Mrufaniwa anaendelea kuwa Mgombea Udiwani katika Kata ya Nsalaga.	*1. Fomu ya uteuzi Namba 8C ya mrufaniwa imegongwa muhuri wa katibu wa Wilaya ya Mbeya Mjini kwa mujibu wa kanuni ya 25 (c) ya Kanuni za Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015.* *2. Mrufaniwa alijibu pingamizi alilowekewa kwa barua ya tarehe 24 Agosti, 2018.*
5	JIJI LA MBEYA	IWAMBI	HUMPHERY ANDREW NGALLAWA	CCM	ELISHA LOSS MWANDELE	CHADEMA	Rufaa imekataliwa na Mrufaniwa anaendelea kuwa Mgombea Udiwani katika Kata ya Iwambi	*Tume imepitia Fomu ya uteuzi ya Mrufaniwa na kujiridhisha kuwa kipengele C cha Fomu za uteuzi kimejazwa kikamilifu na kugongwa muhuri wa Katibu Wilaya ya Mbeya Mjini wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo, kwa mujibu wa kanuni ya 25 ya Kanuni za Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015.*
6	JIJI LA DODOMA	KIZOTA	BANGABABO OMARY HAMISI	CHADEMA	JAMAL PAUL YARERD NGALYA	CCM	Rufaa imekataliwa na mrufaniwa anaendelea kuwa Mgombea Udiwani katika Kata ya Kizota	*1.Vielelezo vilivyowasilishwa vimethibitisha kuwa majina ya Mrufaniwa ni halisi. Aidha, imethibitishwa kupitia barua yenye Kumb Na. AB. 38/375/01/128 ya tarehe 26 Agosti, 2015 kutoka Ofisi ya Msajili wa Vizazi na Vifo kuwa cheti cha kuzaliwa cha Mrufaniwa kilichowasilishwa kuhusiana na majina ya Mrufaniwa siyo halali, hivyo hakiwezi kutumika kama uthibitisho wa jina la Mrufaniwa.* *2. Nakala ya Fomu Namba 10 ya kuheshimu na kutekeleza Maadili ya Uchaguzi iliyoambatishwa na Mrufaniwa imejazwa kwa ukamilifu.* *3. Katika fomu ya uteuzi ya Mrufaniwa amejaza kuwa kazi yake ni mkandarasi mdogo wa majengo/barabara, Aidha, Mrufani hajawasilisha kielelezo chochote kuthibitisha hoja yake.*
7	WILAYA YA MEATU	MWANHUZI	SAMWEL SASABO MAGINA	CHADEMA	ZACHARIA PHILIP MAYOMBI	CCM	Rufaa imekubaliwa na Mrufani amerejeshwa katika orodha ya Wagombea Udiwani katika Kata ya Mwanhuzi.	*1.Tume imefanya rejea katika Kanzidata yake na kujiridhisha kuwa Wapiga Kura waliomdhamini Mrufaniwa wameandikishwa kwenye Daftari la Kudumu la Wapiga kura katika Kata ya Mwanhuzi.*

Na	HALMASHAURI	KATA	MRUFANI		MRUFANIWA		MAAMUZI YA TUME	*SABABU*
			JINA	CHAMA	JINA	CHAMA		
								2.Kwa mujibu wa Kanuni ya 34 ya Kanuni za Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015, Kampeni za Uchaguzi huanza mara baada ya uteuzi na kuisha siku moja kabla ya Uchaguzi. Hivyo, makosa yoyote yanayotendeka kabla ya kipindi cha uteuzi, kampeni, upigaji kura na baada ya kutangaza matokeo yapo chini ya mamlaka nyingine.
8	WILAYA YA MEATU	MWANHUZI	SAMWEL SASABO MAGINA	CHADEMA	ZACHARIA PHILIP MAYOMBI	CCM	Rufaa imekataliwa na Mrufaniwa anaendelea kuwa katika orodha ya Wagombea Udiwani katika Kata ya Mwanhuzi.	*Fomu Na. 12 ya rufaa uliyowasilisha haijaambatishwa na Fomu Na. 9C ya pingamizi pamoja na uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi ambao unakatiwa rufaa kwa mujibu wa Kanuni ya 28 (3) na (6) ya Kanuni za Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2015. Hivyo, Rufaa iliyowasilishwa imekosa sifa za kuwa rufaa.*